**TAARIFA KWA UMMA**

Tume ya Kuchunguza Matukio ya Uvunjifu wa Amani yaliyotokea Wakati na Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025 inapenda kuwafahamisha wananchi wote kwamba imeanza rasmi utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Tume za Uchunguzi, Sura ya 32.

Mafanikio ya Tume yatategemea sana ushirikiano wa kila mwenye taarifa inayoweza kusaidia kujua ukweli. Hivyo, Tume inawaalika wananchi wote, Asasi za Kiraia, viongozi wa dini, vyama vya siasa, makundi ya vijana, na wadau wengine wote kutoa taarifa, ushahidi, maoni, na mapendekezo yatakayoisaidia Tume katika uchunguzi.

Aidha, taarifa, zikiwa katika mfumo wa nyaraka za maandishi; picha (mnato na mjongeo); na vielelezo vingine zitapokelewa kwa njia mbalimbali, ikiwemo: majadiliano/mahojiano ya ana kwa ana; mawasilisho ya maandishi (*written submissions*) kwa njia ya posta au tovuti maalumu ya Tume; barua pepe; ujumbe mfupi wa simu (*SMS*); dodoso maalumu, na mitandao ya kijamii.

Tume itahifadhi usiri kwa watoa taarifa ambao hawatapenda kujulikana na wengine nje ya Tume.

Kwa mawasiliano, tafadhali tumia njia zifuatazo:

**Sanduku la Barua:**
Tume ya Uchunguzi wa
Matukio ya Uvunjifu wa
Amani Wakati na Baada
ya Uchaguzi Mkuu
Oktoba 2025,
S.L.P 471,
Dar Es Salaam.
**Tovuti:** www.tume.uchunguzi.go.tz
**Baruapepe:** maoni@tume.uchunguzi.go.tz, tume.uchunguzi@gmail.com
**Ujumbe mfupi wa Simu/ Whatsapp** – 0743 040890, 0737 305449
**Mitandao ya kijamii** (*Instagram, x*) – tume_uchunguzi

**Imetolewa na**
**MWENYEKITI WA TUME**